TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MATOKEO YA OPERESHENI YA UKAGUZI WA DAWA BANDIA ILIYOTOLEWA NA MKURUGENZI WA UPELELEZI WA MAKOSA YA JINAI CP ROBERT MANUMBA

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Chakula na Dawa Bibi Margareth Ndomondo-Sigonda,

Mwakilishi wa INTERPOL Bi Aline Planc'on

Mkurugenzi Mkuu, Tume ya Ushindani (FCC)

Mkurugenzi Mkuu, Bohari ya Madawa (MSD)

Wakurugenzi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa

Wawakilishi wa INTERPOL SRB Nairobi na SRB Harare

Wanahabari

Wafanyakazi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa

Mabibi na Mabwana,

Awali ya yote napenda kuwashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kipekee niweze kuongea na vyombo vya habari kuhusu operesheni iliyofanyika mfululizo kwa siku sita zilizopita ili kubaini na kukamata dawa bandia hapa nchini.

Kama ilivyoelezwa na Mkurugenzi Mkuu wa TFDA, operesheni hii ililenga mikoa minne (4) ambayo ni Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na Mwanza. Mikoa hii imechaguliwa kutokana na umuhimu wake

kibiashara na pia kwa kuwa ni mikoa ya mipakani. Vile vile Jeshi la Polisi limeendesha operesheni kama hii katika mikoa mingine hapa nchini.

Ndugu wanahabari,

Utekelezaji wa operesheni hii ulitanguliwa na vikao vya maandalizi vilivyohusisha kamati maalamu iliyoundwa kutoka taasisi zilizotajwa hapo awali. Kabla ya operesheni, yalifanyika mafunzo maalum kwa siku mbili kuanzia tarehe 22-23 Septemba 2008 kwa lengo la kuelimisha mbinu na utaratibu wa kuendesha operesheni hii. Jumla ya waendesha operesheni 56 kutoka mikoa hii minne walipata mafunzo hayo. Maofisa hao walitoka katika idara za Polisi, Ushuru na Forodha, Shirika la Viwango, Tume ya Ushindani, Ofisi ya Rais, Bohari ya Madawa na Mamlaka ya Chakula na Dawa.

Maeneo yaliyokaguliwa katika operesheni hii yalitokana na taarifa za awali za kiinteligensia, taarifa kutoka kwa raia wema na uzoefu wa TFDA katika kaguzi zilizopita. Kama ilivyoelezwa hapo awali, operesheni imefanyika kuanzia tarehe 29 Septemba na kumalizika tarehe 4 Oktoba 2008 ambapo leo hii tumeona ni vyema tutoe taarifa kwa umma kupitia wanahabari.

Ndugu wanahabari, katika kujipanga vizuri kwa ajili ya zoezi hili, waendesha operesheni walikuwa wakikutana kila siku jioni kwa lengo la kupeana matokeo ya operesheni, kufanya tathmini na kupanga taratibu za operesheni kwa siku inayofuata. Muda wa operesheni ulikuwa ni kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni. Aidha, Operesheni ilifanyika kwa kuzingatia kanuni na sheria za nchi.

Ndugu wanahabari,

Katika operesheni hii, jumla ya Famasi 69, Maghala ya kutunzia dawa 5, Maduka ya dawa baridi 103 na sehemu zilizotiliwa mashaka 14 zilikaguliwa. Mchanganuo wa kimikoa ni kama ifuatavyo;

Na	**Mkoa**	**Idadi ya sehemu zilizokaguliwa**				
		Famasi	**Maghala ya dawa**	**Duka la Dawa Baridi**	**Hospitali**	**Maeneo mengine**
1	Dar es Salaam	52	5	44	-	3
2	Mbeya	6	-	22	-	-
3	Arusha	3	-	-	2	-

4	Mwanza	5	-	13	-	11*
5	Mikoa mingine	3	-	24	-	-
Jumla		**69**	**5**	**103**	**2**	**14**

*** Mabasi ya Abiria**

Aidha, aina mbalimbali za dawa zilikamatwa kama ifuatavyo;

s/n	**Mkoa**	**Aina za dawa bandia**	**Aina za dawa zilizoisha matumizi**	**Aina za dawa za serikali**	**Aina za dawa zisizosajiliwa**
1	Dar es Salaam	8	15	14	53
2	Mbeya	-	3	-	-
3	Arusha	-	-	3	2
4	Mwanza	1	-	2	2
	Jumla	**9**	**18**	**19**	**57**

Ndugu wanahabari,

Mchanganuo wa dawa bandia zilizokamatwa ni kama ifuatavyo;

a) Dawa ya malaria aina ya Coartem na Duo- Cotecxin
b) Dawa za kutibu ugonjwa wa moyo aina ya Atenolol na Zestril
c) Dawa ya fungus SAFI krimu
d) Dawa ya vitamini mchanganyiko iitwayo Neuroton tablets
e) Dawa ya kurekebisha homoni za akina mama aina ya Primolut -N
f) Dawa ya ugonjwa wa ngozi aina ya Penex krimu na Movelisin gel

Dawa nyingine ni pamoja na dawa za mifugo aina mbalimbali zilizokamatwa kwa kuhisiwa kuwa ni bandia kutokana na ufungashaji hafifu, mtengenezaji kutosajiliwa na TFDA na pia lebo zake kutokukidhi masharti ya sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003. Dawa hizo ni jumla ya boksi 233 yenye paketi kati ya 100 -250.

Jumla ya aina 17 za vipodozi vilivyopigwa marufuku vimekamatwa katika maduka 3.

Matokeo mengine ni pamoja na maduka ya dawa baridi kukutwa kuuza dawa moto zisizoruhusiwa katika maduka hayo, maduka kutokuwa na vibali, uhifadhi hafifu husasan ukosefu wa viyoyozi na wataalam kutokuwa na sifa zinazostahili.

Ndugu wanahabari,

Jumla ya majalada 44 ya kesi yamefunguliwa katika viuto vya Polisi katika mikoa ya Mbeya, Rukwa, Mwanza, Tanga na Dar es Salaam na watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

Aidha, vielelezo pamoja na dawa zilizokamatwa vimehifadhiwa Mamlaka ya Chakula na Dawa na uchunguzi wa kitalaam unaendelea hususan kwa dawa zinazodhaniwa kuwa bandia.

Katika operesheni hii, Maduka ya dawa (Pharmacy) manne (4) na maduka ya dawa baridi 18 yamefungwa kwa kukiuka kanuni za uendeshaji wa maduka hayo. Makosa hayo ni pamoja na kutokuwa na vibali halali vya kuendesha biashara ya dawa, kutokuwa na wataalamu na utunzaji hafifu wa kumbukumbu na dawa.

Ndugu wanahabari,

Operesheni hii imekumbana na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo;

a. Kukosa ushirikiano na baadhi ya wamiliki na wasimamizi wa maeneo ya biashara za dawa.
b. Operesheni kuangukia sikukuu ya mwezi mtukufu wa Ramadhani na hivyo maduka mengi kufungwa kwa siku mbili.
c. Ugumu wa kufahamu vyanzo vya dawa bandia ambapo kunahitaji upelelezi wa kina.
d. Ufinyu wa bajeti katika kuendesha operesheni

Ndugu wanahabari,

Kutokana na matokeo ya operesheni hii, ninapenda kuwahakikishia wananchi kwamba ubora na usalama wa dawa hapa nchini unadhibitiwa ipasavyo. Aidha tunatoa wito na kuwaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa za wote wanaojihusisha na biashara haramu ya dawa bandia kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa na vyombo vya usalama ili waweze kuchukuliwa hatua.

Hivyo, napenda kutoa onyo kali kwa wale wote wanaojihusisha na biashara ya dawa bandia na bidhaa nyingine zozote bandia kuacha mara moja biashara hizo. Ninapenda kuwafahmisha kuwa Jeshi la Polisi pamoja na taasisi za udhibiti wa vyakula, dawa na vipodozi tumejipanga vyema kuwabaini na kuwachukulia hatua kali za kisheria wote watakaobainika kujihusisha na biashara haramu ya dawa bandia.

Vile vile tunaagiza kwamba biashara zote za vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba zisimamiwe na kuendeshwa kitaalam kwa kuzingatia misingi ya sheria na taratibu zilizopo.

Ndugu wanahabari,

Napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa taasisi zilizofanikisha operesheni hii hususan INTERPOL kwa kukubali kushiriki na pia kugharamia kwa kiasi kikubwa operesheni hii. Aidha ninazishukuru taasisi nyingine za Serikali zilizochangia gharama za operesheni hii, ambazo ni Mamlaka ya Chakula na Dawa, Tume ya Ushindani, Bohari ya Madawa (MSD) na Ofisi ya Rais.

Mwisho ninapenda kuwashukuru wananchi wote waliotoa taarifa na pia kuwapongeza wote waliosimamia na kuendesha zoezi hii kwa mafanikio makubwa.

Ahsanteni kwa kunisikiliza